

KUMB: PPR/19 - 04/1

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI
KUANZIA JUMATANO, TAREHE 3 APRILI 2019

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 3 Aprili 2019**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya **Dar es Salaam**, zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 6 Machi 2019. Kuhusu Mafuta ya Taa, bei za jumla na rejareja hazijabadilika kwa sababu hakuna shehena mpya ya mafuta hayo iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam kwa mwezi Machi 2019. Kwa mwezi Aprili 2019, bei za rejareja za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 49/lita (sawa na asilimia 2.34) na Shilingi 61/lita (sawa na asilimia 2.87), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 49.03/lita (sawa na asilimia 2.48) na Shilingi 60.86/lita (sawa na asilimia 3.03), mtawalia. Kwa kiasi kikubwa, mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la ndani kwa mafuta yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam yanatokana na ongezeko la bei za mafuta katika soko la dunia kama inavyoonekana katika **Jedwali C**.
- (b) Hakuna shehena ya mafuta iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya **Tanga** katika mwezi wa Machi 2019 hivyo, bei za mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa kwa **Mikoa ya Kaskazini** zitaendelea kuwa zile za mwezi Machi 2019. Hata hivyo, kuna ongezeko la Shilingi 0.83/lita kwenye bei ya Petroli na Shilingi 0.91/lita kwenye ya Dizeli kutokana na marekebisho ya gharama za uchelewaji wa meli bandarini.
- (c) Vilevile, hakuna shehena ya mafuta iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya **Mtwara** mwezi wa Machi 2019 hivyo, bei za mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa kwa **Mikoa ya Kusini** zitaendelea kuwa kama zilivyokuwa mwezi Machi 2019. Kwa kuwa hakuna Mafuta ya Taa katika ghala za mafuta zilizopo mkoani Mtwara, wamiliki wa vituo vya mafuta katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa mikoa hiyo zinatokana na gharama za mafuta hayo kutokea Dar es Salaam na kusafirishwa hadi mkoa husika.
- (d) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (e) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau

kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

- (f) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*) kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 163 la mwezi Aprili 2018 na Gazeti la Serikali Na. 269 la mwezi Juni 2018.****
- (g) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (h) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
Dar es Salaam	2,147	2,192	2,096
Arusha	2,192	2,196	2,286
Arumeru (Usa West)	2,192	2,196	2,286
Karatu	2,210	2,214	2,304
Longido	2,203	2,207	2,297
Monduli	2,197	2,201	2,291
Monduli-Makuyuni	2,202	2,206	2,296
Ngorongoro (Loliondo)	2,276	2,281	2,371
Pwani (Kibaha)	2,151	2,196	2,101
Bagamoyo	2,158	2,203	2,107
Chalinze Junction	2,161	2,206	2,111
Chalinze (Msata)	2,165	2,210	2,115
Kibiti	2,167	2,212	2,117
Kisarawe	2,154	2,199	2,104
Mkuranga	2,157	2,201	2,106
Rufiji	2,175	2,219	2,124
Dodoma	2,206	2,250	2,155
Bahi	2,213	2,258	2,162
Chamwino	2,201	2,246	2,150

Chemba	2,232	2,277	2,182
Kondo	2,239	2,283	2,188
Kongwa	2,203	2,248	2,152
Mpwapwa	2,207	2,252	2,156
Mtera (Makatopora)	2,225	2,269	2,174
Geita	2,312	2,357	2,262
Bukombe	2,301	2,346	2,251
Chato	2,333	2,378	2,283
Mbogwe	2,351	2,395	2,300
Nyang'hwale	2,327	2,372	2,277
Iringa	2,211	2,256	2,161
Ismani	2,216	2,261	2,166
Kilolo	2,216	2,260	2,165
Mufindi (Mafinga)	2,221	2,266	2,171
Kagera (Bukoba)	2,363	2,407	2,312
Biharamulo	2,337	2,382	2,286
Karagwe (Kayanga)	2,379	2,424	2,328
Kyerwa (Ruberwa)	2,385	2,429	2,334
Muleba	2,363	2,407	2,312
Ngara	2,350	2,395	2,300
Misenyi	2,371	2,416	2,320
Katavi (Mpanda)	2,355	2,400	2,304
Mlele (Inyonga)	2,337	2,382	2,286
Mpimbwe (Majimoto)	2,347	2,392	2,297
Kigoma	2,378	2,423	2,328
Uvinza (Lugufu)	2,391	2,435	2,340
Buhigwe	2,368	2,412	2,317
Kakonko	2,335	2,380	2,285
Kasulu	2,364	2,409	2,314
Kibondo	2,343	2,387	2,292
Kilimanjaro (Moshi)	2,181	2,186	2,276
Hai (Bomang'ombe)	2,185	2,189	2,279
Mwanga	2,175	2,179	2,269
Rombo (Mkuu)	2,198	2,202	2,292
Same	2,168	2,172	2,262
Siha (Sanya Juu)	2,188	2,192	2,282
Lindi	2,141	2,236	2,155
Lindi-Mtama	2,146	2,240	2,173
Kilwa Masoko	2,165	2,259	2,130
Liwale	2,177	2,271	2,176
Nachingwea	2,161	2,256	2,185
Ruangwa	2,167	2,262	2,186
Manyara (Babati)	2,226	2,230	2,320
Hanang (Katesh)	2,236	2,241	2,331
Kiteto (Kibaya)	2,241	2,245	2,335
Mbulu	2,239	2,243	2,333
Simanjiro (Orkasumet)	2,258	2,262	2,352
Mara (Musoma)	2,326	2,370	2,275

Musoma Vijijini (Busekela)	2,366	2,411	2,316
Rorya (Ingirijuu)	2,334	2,379	2,284
Rorya (Shirati)	2,369	2,414	2,319
Bunda	2,317	2,361	2,266
Butiama	2,322	2,367	2,272
Serengeti (Mugumu)	2,371	2,416	2,321
Tarime	2,337	2,381	2,286
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,341	2,386	2,291
Mbeya	2,254	2,299	2,204
Chunya	2,264	2,308	2,213
Chunya (Makongolosi)	2,278	2,323	2,227
Kyela	2,270	2,315	2,219
Mbarali (Rujewa)	2,238	2,283	2,188
Rungwe (Tukuyu)	2,263	2,308	2,213
Morogoro	2,172	2,217	2,121
Mikumi	2,188	2,232	2,137
Kilombero (Ifakara)	2,210	2,255	2,159
Kilombero (Mlimba)	2,232	2,277	2,182
Kilombero (Mngeta)	2,221	2,266	2,171
Ulanga (Mahenge)	2,220	2,265	2,170
Malinyi	2,231	2,275	2,180
Kilosa	2,190	2,235	2,140
Gairo	2,190	2,235	2,140
Mvomero (Wami Sokoine)	2,182	2,227	2,132
Turiani	2,197	2,242	2,146
Mtwara	2,127	2,222	2,169
Nanyumbu (Mangaka)	2,164	2,258	2,218
Masasi	2,144	2,238	2,195
Newala	2,148	2,243	2,201
Tandahimba	2,141	2,236	2,194
Nanyamba	2,141	2,236	2,194
Mwanza	2,297	2,342	2,247
Kwimba	2,315	2,360	2,264
Magu	2,305	2,350	2,255
Misungwi	2,292	2,336	2,241
Sengerema	2,330	2,374	2,279
Ukerewe	2,357	2,401	2,306
Njombe	2,239	2,284	2,189
Njombe (Kidegembye)	2,260	2,305	2,209
Ludewa	2,277	2,322	2,227
Makambako	2,232	2,276	2,181
Makete	2,270	2,315	2,220
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,237	2,282	2,187
Rukwa (Sumbawanga)	2,320	2,365	2,269
Sumbawanga Rural (Mtowisa)	2,320	2,365	2,269
Kalambo (Matai)	2,327	2,372	2,277
Nkasi (Namanye)	2,333	2,378	2,283
Ruvuma (Songea)	2,213	2,308	2,220

Mbinga	2,226	2,320	2,253
Namtumbo	2,204	2,299	2,249
Nyasa (Mbamba Bay)	2,251	2,346	2,264
Tunduru	2,178	2,273	2,279
Shinyanga	2,276	2,321	2,225
Kahama	2,290	2,334	2,239
Kishapu	2,304	2,349	2,254
Ushetu (Nyamilangano)	2,307	2,352	2,257
Simiyu (Bariadi)	2,317	2,362	2,267
Busega (Nyashimo)	2,310	2,355	2,260
Itilima (Lagangabilili)	2,320	2,365	2,270
Maswa	2,309	2,354	2,258
Meatu (Mwanhuzi)	2,316	2,361	2,265
Singida	2,238	2,282	2,187
Iramba	2,250	2,295	2,199
Manyoni	2,222	2,267	2,172
Ikungi	2,233	2,278	2,183
Mkalama (Nduguti)	2,262	2,307	2,212
Songwe (Vwawa)	2,263	2,308	2,213
Songwe (Mkwajuni)	2,270	2,315	2,220
Ileje	2,267	2,312	2,217
Momba (Chitete)	2,272	2,317	2,222
Tunduma	2,268	2,312	2,217
Tabora	2,301	2,346	2,251
Igunga	2,255	2,300	2,205
Kaliua	2,320	2,365	2,270
Ulyankulu	2,314	2,359	2,264
Nzega	2,266	2,310	2,215
Sikonge	2,313	2,358	2,262
Urambo	2,314	2,359	2,264
Uyui	2,302	2,347	2,252
Tanga	2,135	2,139	2,229
Handeni	2,156	2,160	2,250
Kilindi	2,171	2,175	2,265
Korogwe	2,147	2,151	2,241
Lushoto	2,157	2,161	2,251
Mkinga (Maramba)	2,142	2,146	2,236
Muheza	2,140	2,144	2,234
Pangani	2,142	2,146	2,236

JEDWALI B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,023.19	2,067.44	1,973.03

Bei za Jumla - TANGA	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
----------------------	---------	--------	---------------

	(Shs/Lita)	(Shs/Lita)	(Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,011.45	2,015.26	2,105.56

Bei za Jumla - MTWARA	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,003.80	2,097.85	-----

JEDWALI C: SABABU ZA MABADILIKO YA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI

BANDARI YA DAR ES SALAAM

	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia	Ongezeko la Dola 46.842/Tani	Ongezeko la Dola 66.434/Tani	----
Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums)	Punguzo la Dola 20.220/Tani	Punguzo la Dola 4.322/Tani	----

JEDWALI D: BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA DUNIA ZILIZOTUMIKA KUKOKOTOA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI

	Bandari	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Mafuta yalipokelewa mwezi wa:	DSM	Machi 2019	Machi 2019	Februari 2019
	Tanga	Februari 2019	Februari 2019	Desemba 2018
	Mtwara	Februari 2019	Februari 2019	----
Wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa mwezi:	DSM	Februari 2019	Februari 2019	Januari 2019
	Tanga	Januari 2019	Januari 2019	Novemba 2019
	Mtwara	Januari 2019	Januari 2019	----

Nzinyangwa E. Mchany
KAIMU MKURUGENZI MKUU
EWURA